



TAARIFA KWA WANAHISA WA BENKI YA BIASHARA MKOMBOZI

TAARIFA INATOLEWA KWAMBA, Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu wa Wanahisa wa Benki ya Biashara Mkombozi utafanyika siku ya Jumamosi, tarehe 30 Julai 2022, kwenye ukumbi wa Ubungo Plaza, jijini Dar es Salaam, kuanzia saa 3.00 asubuhi.

AJENDA

- 13.1 Kufungua mkutano;
- 13.2 Kuridhia ajenda za mkutano;
- 13.3 Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili wa mwaka uliofanyika tarehe 31 Julai 2021;
- 13.4 Kupokea na kujadili yatokanayo na taarifa ya Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili wa mwaka uliofanyika tarehe 31 Julai 2021;
- 13.5 Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2021;
- 13.6 Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya fedha ya Benki kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021; na kupokea taarifa ya Mbaguzi wa nje wa hesabu, juu ya taarifa hiyo ya fedha.;
- 13.7 Kuteua Mbaguzi wa nje wa hesabu za Benki;
- 13.8 Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa mwaka ujao;
- 13.9 Mengineyo; na
- 13.10 Kufunga Mkutano

ANGALIZO

1. Mwanahisa anayetaka kushiriki katika mkutano huu ni lazima awasilishe nakala ya risiti yake ya ununuzi wa hisa, cheti cha hisa cha kumtambulisha kuwa ni mwanahisa au kitambulisho chochote kinachotambulika.
2. Mwanahisa mwenye stahili ya kuhudhuria mkutano huu ana haki ya kumteua mwakilishi wake wa kupiga kura kwa niaba yake kwa mujibu wa taratibu za kampuni. Fomu husika inayopaswa kujazwa na Mwanahisa kwa ajili ya uteuzi huo inatakiwa kufikishwa kwa katibu wa Benki siku tatu kabla ya mkutano. Fomu hiyo iandikwe kama ifuatavyo: -

"Benki ya Biashara Mkombozi"

Mimi/Sisi....., wa, nikiwa/
tukiwa Mwanahisa/Mjumbe wa Kampuni iliyotajwa hapo juu, namteua/ tunamteua
..... wa
kama mwakilishi wangu/wetu kupiga kura kwa niaba yangu/ yetu katika Mkutano Mkuu
wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki utakaofanyika tarehe 30 Julai, 2022.

Imesainiwa, leo tarehe Mwezi2022

3. Wanahisa wote au wawakilishi wao watasajiliwa kabla ya kuingia kwenye ukumbi wa mkutano siku hiyo.
4. Vitabu vya taarifa ya Mkutano wa kumi na tatu (13) wa Wanahisa vitakuwepo katika matawi ya Benki wiki mbili kabla ya mkutano.
5. Nakala laini za vitabu vya Mkutano wa kumi na tatu (13) wa Wanahisa vimeshawekwa kwenye tovuti ya Benki.
6. Fulana kwa ajili ya Wanahisa zitapatikana katika matawi ya Benki yaliyopo Dar es salaam wiki mbili kabla ya mkutano.
7. Kwa maoni kabla ya siku ya mkutano tafadhali tuma ujumbe kwenye anwani yetu ya barua pepe info@mkombozibank.co.tz au kwenda namba yetu ya WhatsApp : 0754 236 766

Kwa taarifa zaidi fika:
Benki ya Biashara Mkombozi,
Kitalu Na. 40, Nyuma ya Kanisa la Mt. Joseph,
Mtaa wa Mansfield,
S.L.P. 38448,
DAR ES SALAAM.
Namba za simu: +255 22 2137806/7
Namba ya bure ya maulizo: 0800 750 040
Barua Pepe: info@mkombozibank.co.tz

OSWARD LESLIE MPANGALA
MENEJA HUDUMA ZA SHERIA
KWA MAELEKEZO YA BODI YA WAKURUGENZI
JUNI, 2022